


SANVN VIWANDA SCHAME

SANVN viwanda Schame ni mpango wa uwezesajî wananchi kiuchumi ili kutatua changamoto ya upatikanaji wa ujuzi, masoko na mitaji katika miradi midogo na ya kati (SMI). Walengwa wa Mpango huu ni Wajasiriamali wadogo na wa kati wenye viwanda wanaojishughulisha katika kuzalisha bidhaa ili kuongeza mnyororo wa thamani . Mpango huu unaratibiwa na taasisi tano (05) ambazo ni SIDO, AZANIA BANK, NSSF, VETA na NEEC.



SANVN VIWANDA SCHEME

SANVN VIWANDA SCHAME

UCHUMI WA VIWANDA

**WANAOKIDHI VIGEZO
WATEMBELEE OFISI ZA SIDO
MKOA AU VETA KWA AJILI YA
KUSHUGHULIKIA UPATIKANAJI
WA MIKOPO HII ZILIZOPO
NZIMA**



SIFA ZA MWOMBAJI

SIFA ZA UJUMLA

1. MWOMBAJI LAZIMA AWE NA UMRI USIOPUNGUA MIAKA 18 NA AWE RAIA WA TANZANIA .
2. MRADI LAZIMA UWE UMESAJIJIWA KISHERIA , UMEFANYIWA UPEMBUZI AKINIFU WA KIFEDHA NA UNAKUBALIKA KIJAMII
3. MRADI NI LAZIMA UWE WA UZALISHAJI BIDHAA (KIWANDA) NA KUENDESHWA KWA KIPINDI KISICHOPUNGUA MWAKA MMOJA (01) (VIWANDA VINAVYOONGEZA THAMANI MAZAO YA KILIMO VINAPEWA KIPAUMBELE)
4. MWOMBAJI AWE ANAKUSUDIA KUANZISHA KIWANDA KWA SHARTI LA KUWA NA VYANZO VINGINE VYA MAPATO KUPITIA AJIRA , BIASHARA, KILIMO AU NYINGINE INAYOWEZA ONYESHA UWEZO WA KUREJESHA MKOPO UNAOHITAJI
5. MWOMBAJI LAZIMA AWE MNUFAIKA WA HUDUMA ZA SIDO AU VETA
6. MWOMBAJI AWE MWANACHAMA WA NSSF AU AWE TAYARI KUJIUNGA UANACHAMA
7. AWE NA DHAMANA YENYE THAMANI YA 125% YA KIWANGO CHA MKOPO . KWA MKOPO WA MASHINE/ MITAMBO YA UZALISHAJII, MKOPAJI ATALIPIA 20% YA GHARAMA YA MASHINE/MITAMBO NA MKOPO UTALIPA 80% NA MASHINE/MTAMBO HUSIKA UTAKUWA DHAMANA YA MKOPO.
8. MIKOPO YA VIKUNDI HUTOLEWA KWA VIKUNDI VYENYE WATU KATI YA 5 NA 15 VILIVYOUNDWA NA SIDO AU VETA KUPITIA PROGRAM ZA MAFUNZO.

AINA ZA MIKOPO

SANVN VIWANDA SCHEME INATOA MIKOPO KWA AJILI YA UWEZESHAI MIRADI YA UZALISHAJI (VIWANDA) KWA KIASI CHA KATI YA SHILINGI MILIONI 8 HADIL MILIONI HAMSINI (50 MIL) KWA WAJASIRIAMALI WADOGO. WAJASIRIAMALI WA KATI NI MILIONI HAMSINI (50 MIL) HADIL MILIONI MIA TANO (500MIL). MIKOPO YA SANVN IMEGAWANYIKA KATIKA MAKUNDI YAFUATAYO;

1. MIKOPO YA UWEKEZAJI/MASHINE, MITAMBO, (INVESTMENT LOAN)

MIKOPO YA UWEKEZAJI NI MIKOPO ITOLEWAYO KWA AJILI YA UNUNUZI WA MASHINE/MITAMBO ILI KUANZISHA/KUENDELEZA VIWANDA VIDOGO AU VYA KATI (SMI)

VIGEZO NA MASHARTI

- * MUDA WA UREJESHAJI NI KATI YA MWAKA 1-3
- * KIASI CHA MKOPO NI KATI YA MILIONI NANE (8 MIL) NA MILIONI MIA TANO (500 MIL)
- * MKOPO WA 80% YA THAMANI YA MASHINE HUTOLEWA
- * UTHIBITISHO WA MKATABA WA UPANGAJI AU UMILIKI WA ENEO ITAKAPOFUNGWA MASHINE
- * FEDHA YA MKOPO ITALIPIA MASHINE MOJA KWA MOJA KWA MUUZAJI
- * UTHIBITISHO WA HUDUMA ULIYOPATIWA NA SIDO AU VETA
- * RIBA YA 13% ITATOZWA KWA MWAKA (RIBA ITATATOZWA KWENYE SALIO LA MKOPO)
- * KIKUNDI CHA WATU 5-10 KINATAKIWA KUWA NA BARUA YA UTAMBULISHO TOKA TAASISI INAYOWASIMAMIA KWA MAANA YA SIDO AU VETA
- * BIMA YA MKOPO NI ASILIMIA MBILI (02) YA KIWANGO CHA MKOPO NA HUTOZWA MARA MOJA.

1. MIKOPO ISIYO

YAKIUWEKEZAJI (WORKING CAPITAL LOAN)

HII NI MIKOPO ITOLEWAYO KWA LENGO LA KUWEZESA SHUGHULI ZA KIUTENDAJI ZA KILA SIKU MFANO UNUNUZI WA MALIGHAFI, VIFUNGASHIO, MATANGAZO NA GHARAMA ZINGINE ZA UENDESHAJI

VIGEZO NA MASHARTI

- * MUDA WA UREJESHAJI NI KATI YA MWAKA 1-3
- * KIASI CHA MKOPO NI KATI YA MILIONI NANE (8 MIL) NA MILIONI MIA TANO (500 MIL)
- * DHAMANA YA MKOPO IWE NA THAMANI YA 125% YA MKOPO (HATI ZILIZOSAJILIWA NA ZISIZOSAJILIWA KWA KUDHINGATIA KIWANGO CHA MKOPO NA ENEO DHAMANA ILIPO).
- * UTHIBITISHO WA MKATABA WA UPANGAJI AU UMILIKI WA ENEO LA MRADI
- * UTHIBITISHO WA HUDUMA ULIYOPATIWA NA SIDO AU VETA
- * RIBA YA 13% ITATOZWA KWA MWAKA (RIBA ITATATOZWA KWENYE SALIO LA MKOPO)
- * KIKUNDI CHA WATU 5-10 KINATAKIWA KUWA NA BARUA YA UTAMBULISHO TOKA TAASISI INAYOWASIMAMIA KWA MAANA YA SIDO AU VETA
- * BIMA YA MKOPO NI ASILIMIA MBILI (02) YA KIWANGO CHA MKOPO NA HUTOZWA MARA MOJA.